

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

Telegrams: "MSW"
Telephone: + 028 2750271
Fax: + 028 2750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz



S.L.P 170,
MASWA,
SIMIYU.

Kumb.Na. MDC/ADM/10/30/VOL 1/85

03 JANUARI,2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kupitia kibali cha ajira mbadala **Kumb. Na.FA.170/533/01"B"/65** cha tarehe **26 Novemba 2021**, kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inatangaza nafasi wazi moja [1] ya Mtendaji wa kijiji Daraja la III na Dereva Daraja la II.

1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA II – NAFASI 1

1.1. Sifa za Mwombaji:-

- Wahitimu wa kidato cha nne au sita wenye cheti cha [NTA Level 5] au Certificate katika moja ya fani zifuatazo.
- Utawala
- Usimamizi wa Rasilimali watu
- Maendeleo ya Jamii au
- Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
 - (iii) Awe na umri usiozidi miaka 45
 - (iv) Awe na cheti cha kuzaliwa.

1.2. MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji,
- (ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- (v) Kutafasiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.
- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- (viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- (ix) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.

- (x) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi.
- (xi) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- (xii) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- (xiii) Kazi nyingine utakayopewa na Mkuregenzi Mtendaji wa Halmashauri.

1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara: Ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

2.0 DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 1

2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- (i) Awe na elimu ya kidato cha IV au VI
- (ii) Awe na leseni daraja la "C"
- (iii) Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajali
- (iv) Awe na umri usiozidi miaka 45
- (v) Awe na cheti cha Majaribio ya Ufundu Daraja la II
- (vi) Awe na cheti cha kuzaliwa

2.2 MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalma wa gari
- (ii) kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- (iii) kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- (iv) kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- (v) kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- (vi) kufanya usafi wa gari
- (vii) kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

2.3. NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara: Ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

3.0. MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji waambatanishe na nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyodhibitishwa na Wakili au Mahakama.

- Muombaji ambatanishe picha mbili [2] ndogo ya rangi [passport size] ya hivi karibuni
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita [form VI and form IV result slip] **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

4.0. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
 Halmashauri ya wilaya ya Maswa,
 S.L.P. 170,
MASWA –SIMIYU.

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 18.01.2021 saa 9.30 alasiri.**

NB:

Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri www.maswadc.go.tz Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz na katika mbao za matangazo za Halmashauri na Mkoa wa Simiyu.



Simon S. Berege
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA